



JAMHURI YA KENYA

WIZARA YA MAZINGIRA NA RASILI MALI MADINI

IDARA YA UTABIRI WA HALI YA HEWA

Dagoretti Kona, Barabara kuu ya Ngong, S.L.P. 30259, 00100 GPO, Nairobi, Kenya

Simu: 254 (0) 20 3867880-7 / 3876957/60 / 3873682

Rununu: 254(0)724255153/ 254(0)724255154

Kipepesi: 254 (0) 20 3876955/3877373/3867888/3874501

Baruapepe: director@meteo.go.ke; Tovuti: <http://www.meteo.go.ke>

Namba ya Kumbukumbu **Met/ 7/23**

Tarehe: **27 Februari, 2009**

Taarifa Kwa Vyombo vya Habari

UTABIRI WA MSIMU WA MVUA ZA MASIKA (MACHI- APRILI-MEI 2010)

1 MUKTASARI

- Msimu huu ulitangulizwa na hali ya joto jingi katika bahari ya Hindi linalohusishwa na El_Nino;
- Magharibi mwa Bahari ya Hindi imeendelea kuwa na hali joto ya juu kuliko kawaida;
- Vimbunga navyo vimekuwepo huko bahari ya Hindi hata kufikia sasa Machi 2010.
- Mwelekeo wa Mvua ya Masika (Machi - Mei) inaonyesha uwezekano kuwa; sehemu kubwa ya Kenya itakuwa na mvua ya kawaida ilihali sehemu za Magharibi, Rift Valley ya Kati na Nyanza huenda kukawa na mvua ya kutosha.
- Mvua ya msimu huu wa Masika yatarajiwa kuwa na vipindi virefu vya ukosefu wa mvua hasa katika sehemu kame (ASALs).

2 Hali ilivyokuwa Katika Kipindi Cha Mvua za Vuli (Oktoba- Novemba- Disemba 2009) na Januari Hadi Februari 2010).

2.1. Oktoba – Novemba – Disemba 2009 (Mvua za Vuli)

Msimu huu uliambatana na hali ya El_Nino (hali ya joto jingi katika bahari ya Pasifiki) ambayo bado ipo hadi wakati huu. Kutokana na hali hiyo ya El-Nino, sehemu nyingi zilipata mvua nyingi ingawaje mgao ulikuwa sio mzuri. Kwani mvua ilinyesha nyingi lakini vipindi vya jua vikawa virefu mno kabla mvua kurudi. Sehemu kama vile Lamu, Malindi, Msabaha na Mtwapa huko pwani; Mandera, Garissa na Wajir mkoa wa Kasikazini Mashariki;Lodwar, Kitale, Nakuru, Kericho na Eldoret mkoa wa Bode la Ufa; na Mkoa wa Kati kama Nyeri zilipata mvua nyingi.

Kwa ujumla, vituo 24 kati ya 33 ambavyo vinatumiwa kuchunguza matukio ya msimu viliripoti mvua zaidi ya kawaida.

2.2. Januari – Februari 2010

Kwa kawaida hiki ni kipindi cha kiangazi katika sehemu nyingi humu nchini. Lakini kunazo sehemu ambazo zilipata mvua. Maeneo kama Narok, Thika, Meru Kakamega, Kericho na Nairobi. Kwingineko hali ilikuwa ya kawaida.

3 Utabiri wa Mvua za Masika (Machi-Mei 2010)

Msimu wa mvua za Masika ni muhimu sana Kenya na katika sehemu zingine za Afrika Mashariki kwa ujumla. Msimu huu wa masika ni wakutegemewa sana katika maeneo ya Magharibi, Nyanza, Rift Valley ya kati, Wilaya za Kati na Nairobi. Kwa kawaida, Mkoa wa Magharibi, Nyanza, Kati na Nairobi hupata mvua ya milimita 400 hadi 680, Mkoa wa Bonde la Ufa hupata mvua ya milimita 90 huko kaskazini hadi kufikia milimita 250 huko kusini mwa mkoa wa bonde la ufa, Mkoa wa Kaskazini Mashariki hupata mvua milimita 140 hadi 250, Mkoa wa Mashariki hupata mvua milimita 190 hadi 390. Nayo Pwani hupata mvua takriban milimita 300 hadi 520. Hivi ni viwango vya kawaida katika msimu wa mvua za Masika.

Katika msimu huu wa mvua za masika, sehemu nyingi nchini zinatarajiwa kupata mvua ya kiwango cha kawaida. Ni Sehemu za mkoa wa Pwani na sehemu chache za mkoa wa Kaskazini Mashariki ambazo zinatarajiwa kupata mvua ya kawaida na kuegemea chini ya kawaida.

Ufuatao ni utabiri kamili kulingana na mikoa (**Angalia mchoro No.1**).

- 3.1 **Mkoa wa Magharibi** (Busia, Butere, Mumias, Vihiga, Kakamega, Bungoma, n.k), **Mkoa wa Nyanza** (Kisumu, Siaya, Migori, Kisii, Kuria, Nyamira, Borabu, Gucha, n.k), na **Rift Valley ya Kati** (Turkana, Pokot, Trans Nzoia, Molo, Kericho, Nandi, Sotik n.k), **Mkoa wa Kati** (Nyandarua, Nyeri, Thika, Murang'a, Kirinyaga, Mwea, Maragua,n.k), **Mkoa wa Nairobi** (Westlands, Embakasi, Kasarani, Dagoretti, n.k), **Mkoa wa Mashariki** (Embu Meru,Tharaka, Imenti, Mwingi, Machakos, Makueni, Kibwezi,etc), **Mkoa wa Kaskazini Mashariki** (Mandera,Wajir, Elwak, Garissa, Ijara n.k) sehemu hizi zatarajiwa kwamba zitapata mvua ya kawaida na hata kuzidi kawaida (mvua ya kutosha).
- 3.2 **Mwambao wa Pwani ya Kaskazini** (Msabaha, Vipingo, Malindi, Lamu, n.k), **Sehemu zingine za Pwani** (Tana River, Taita, Taveta, Voi, Mombasa Kwale, Msabweni, Kinango, Lungalunga, n.k) sehemu hizi zakadiriwa zitapata mvua ya kawaida ikiwa na muelekeo wa chini ya kawaida.

4 Ugavi wa Mvua Kimaeneo

Msimu unatarajiwa kuwa na mgao ambao sio mzuri. Maeneo mengine huenda kukatokea vipindi virefu vya jua kali baada ya mvua kuanza na baadaye kusitisha kabla ya mvua nyingine kunyesha na kuendelea, hasa katika sehemu kame. Wakati huo huo kuna uwezekano wa mvua kuwa kubwa/nzito pindi inaponyesha.

5 Mwanzo na Mwisho wa Msimu wa Mvua ya Masika -Machi-Mei 2010 (Angalia Mchoro No 2a na 2b)

- 5.1 *Mkoa wa Magharibi (Busia, Butere, Mumias, Vihiga, Kakamega, Bungoma, etc), Mkoa wa Nyanza (Kisumu, Bondo, Siaya, Migori, Kisii, Kuria, Nyamira, Borabu, Gucha, n.k), Mvua inatarajiwa kuanza juma la kwanza na la pili Machi kuendelea hadi Juni*
- 5.2 *Kusini mwa Rift Valley (Kajiado, Narok, Ngong, Isinya, Namanga, Loitoktok, n.k), mvua yatarajiwa kuanza juma la pili la mwezi wa Machi na kukatika juma la tatu la mwezi wa Mei.*
- 5.3 *Kusini mwa Mkoa wa Mashariki (Embu, Meru, Tharaka, Imenti, Mwingi, Machakos, Makueni, Kibwezi, etc), Sehemu zingine za Pwani (Tana River, Taita, Taveta, Voi, n.k) mwanzo wa mvua watarajiwa katika juma la tatu la mwezi wa Machi na kukatika juma la tatu la mwezi wa Mei.*
- 5.4 *Kaskazini mwa Rift Valley (Trans Nzoia, Uasin Gishu, n.k) mvua inatarajiwa kuendelea kutoka sasa mwanzo wa Machi na kuendelea hadi mwezi wa Juni.*
- 5.5 *Kaskazini Magharibi (Turkana, Pokot) mvua inatarajiwa kuanza juma la mwisho la mwezi wa Machi na kukatika juma la pili la Mei. Kama mwezi moja unusu.*
- 5.6 *Mkoa wa Kaskazini Mashariki (Garissa, Wajir, Mandera, n.k) pamoja na Kaskazini mwa Mkoa wa Mashariki (Marsabit, Moyale) mvua yatarajiwa kuanza juma la mwisho la mwezi wa Machi/ juma la kwanza la mwezi wa Aprili na kukatika juma la pili la mwezi wa Mei.*
- 5.7 *Nyanda za juu za Mkoa wa Mashariki (Embu, Meru, n.k.), Mkoa wa Kati (Nyeri, Murang'a, Kiambu, n.k.) na Mkoa Nairobi mvua yatarajiwa kuanza juma la tatu la mwezi wa Machi na kuisha katika juma la tatu la Mei.*
- 5.8 *Mwambao wa Pwani ya Kaskazini (Mombasa, Kilifi, Lamu, Malindi Msabaha, Vipingo, Kwale n.k) mvua yabashiriwa kuanza juma la mwisho la mwezi wa Machi/ juma la kwanza la mwezi wa Aprili na kuendelea hadi Juni.*

6 Matarajio ya adhari za Mvua ya Msimu katika Sekta Mbalimbali

6.1 Sekta ya Kilimo na Urahisi wa kupata chakula

Zile sehemu ambazo mvua itakuwa ya kutosha, kama vile Magharibi, Nyanza na Rift Valley (Mkoa wa Bonde la Ufa) wakulima wanashauriwa watumie nafasi hii kuzalisha mazao mengi wakishauriana na maafisa wa kilimo wa nyanjani.

Vilevile, zile sehemu ambazo mvua inatarajiwa kuwa ya kiasi lakini labda msimu kuwa mfupi, kama vile mkoa wa Kati, Mashariki, Pwani na Kaskazini Mashariki wakulima wanashauriwa wafuate maagizo kutoka Wizara ya Kilimo hususan kuhusu aina ya mbegu zinazolingana na kiasi cha mvua. Lishe ya mifugo inatarajiwa kuwa ya kuridhisha.

6.2 Sekta ya Kukabiliana na Majanga

Kutokana na mvua inayotarajiwa huko mikoa ya magharibi, bonde la ufa, na Nyanza, maeneo kama vile Kakamega, Murang'a na Keiyo, wananchi wanashauriwa wajihadhari na maporomoko ya ardhi na radi hasa maeneo ya magharibi mwa Kenya kama vile; Gusii na Kakamega. Budalangi, Kano na maeneo ya Nyando kuna uwezekano wa kutokea mafuriko. Hivyo basi wanoishi sehemu hizo itabidi wajiepushe na adhari za mafuriko. Huenda Mto Tana ukafurika kutokana na mvua nyingi ambayo inatarajiwa maeneo ya Mlima Kenya.

Kitengo cha Kukabiliana na Majanga (National Disaster Operation Centre (NDOC)) kinashauriwa kichukue tahadhari mufti ili kukabiliana na majanga haya.

6.3 Sekta ya Kawi

Sehemu za mito inayopeleka maji kwenye Mabwawa ya kuzalisha umeme (Turkwel na Sondu Miriu) zinatarajiwa kupata mvua ya kutosha kwa hivyo shuguli za uzalishaji wa umeme hazitarajiwi kuadhirika. Mto Tana ambao maji yake huingia mabwawa ya Seven Folks (Masinga Dam, n.k), huenda ikapata mvua ya kutosha. Mipango maalumu yahitajika kufanywa katika shughuli za uzalishaji wa umeme kuambatana na hali ya msimu itakavyojiri.

6.4 Sekta ya Uchukuzi na Usalama wa Uma

Mvua Kubwa ya masaa machache huenda ikatatiza hali ya usafiri hasa katika sehemu za Wilaya za Mikoa ya Kati, Magharibi na Mashariki. Barabara wakati kama huu huwatelezi. Msongamano wa magari mijini utashuhudiwa na madereva kukosa subira. Madereva wanashauriwa wawe waangalifu wakati huu wa msimu wa mvua.

Mida kama hii ya mvua huandamana na uwepo wa mawingu mengi mno na dhoruba kali. Marubani wanahimizwa wachukue tahadhari wanapopaa na ndege hasa kwenye safari za magharibi mwa nchi nyakati za alasiri.

6.5 Sekta ya Maji

Maji kwa matumizi mbalimbali yanatarajiwa kuwa ya kutosha. Watu wanombwa wajaribu kutega na kuhifadhi maji ya mvua ili kupunguza uhaba wake. Lakini mabaraza ya miji yanahimizwa kuwa na mipango kabambe ili wananchi wasipate shida. Ushauri kwa wakaazi wa sehemu zingine za nchi ni kwamba watumie maji kwa uangalifu hasa sehemu zile ambazo mvua inatarajiwa kuwa pungufu na hasa sehemu kame (ASALS).

6.6 Mabaraza ya Miji

Mabaraza ya miji ambayo yako katika sehemu zinazotarajiwa kupata mvua nyingi, yanashauriwa kuzibua mitaro ya kupitisha maji ya mvua mapema ili kuepukana na mafuriko mijini na pia kukwepa kutatiza shughuli za wakaazi wa miji hiyo.

6.7 Sekta ya Afya

Mikurupuko ya magonjwa yanayozuka au kuzidi kutokana na hali ya hewa iwe iwayo huenda yakaongezeka. Visa vya malaria na homa ya matumbo huenda vikaongezeka katika maeneo yenye mafuriko. Wanaoshughulikia sekta hii ya afya, yafaa wachukue tahadhari kwa kuongeza madawa hospitali ili wawe tayari kukabiliana na visa vya magonjwa.

6.8 Sekta ya Viwanda

Matatizo ya kuchelewa kwa magari yanayosafirisha mali huenda yakaibuka kwa sababu ya kukwama ama magari hayo kutofika kabisa. Sekta hii ya viwanda huenda ikaadhirika kwa kukosa malighafi ambayo hutumika kutengeneza bidhaa mbalimbali.

6.9 Mazingira

Watu waliokatika maeneo ambayo yatapata mvua ya kutosha, wanahimizwa kutumia mbinu sambamba ili kuzuia mmomonyoko wa udongo. Huu pia ni wakati mzuri wa kupanda miti, hasa ile ya kienyeji ili kuongeza misitu yetu na kuzuia kupanuka kwa jangwa.


ILANI

Mnaombwa kutumia utabiri huu pamoja na ule unaotolewa kila siku na idara hii kwa kupitia vyombo vya habari na mtandao kwa manufaa zaida.




Dr Joseph R. Mukabana, MBS


MKURUGENZI WA HUDUMA ZA UTABIRI WA HALI YA HEWA



**Mchoro. 1: Utabiri wa Mvua za Masika Machi –
Aprili - Mei 2010.**



**Mchoro2a: Kuanza kwa mvua ya MAM 2010- wiki
kuanzia Machi 2010.**



**Mchoro 2b: Kukatika kwa mvua MAM 2010 –
wiki kuanzia Mei 2010**